STAR OF NEW GENERATION 1
COMPANY
TRANSFORMED MINDSET



# FURAHIA HUDUMA ZETU

**Star of New Generation1 Ltd** ni kampuni pekee inayokupatia huduma bora za Afya ya Akili kwa ustawi wako na hata vizazi baada yako. Karibu ufahamu zaidi kuhusu **PACKAGES** za huduma zetu.

# STAR OF NEW GENERATION1 COMPANY LTD

**Star of New Generation1 Company Limited (SNG1)** ni kampuni ya kwanza Tanzania, Afrika na duniani inayojikita kwenye afya ya akili inayolenga ustawi wa mtu na vizazi kupitia matumizi ya kutambua uwezo unaoacha alama. SNG1 ni kampuni inayotambulika na kusajiliwa rasmi nchini Tanzania ikiwa na **namba ya usajili 171466490**. Malengo ya kampuni hii ni kuhamasisha na kuleta chachu ya mabadiliko ya kifikra kwa watu wote kuwa tayari kutambua, kukubali, kudhihirisha, kutathimini na kuwa na mwendelezo wa matumizi sahihi ya uwezo walionao.

SNG1 ilianzishwa na mtaalamu na mbobezi wa saikolojia, *Baraka T. Adolph Mushobozi* mwaka 2021, na ilianza kama ofisi. Kama mwanzilishi, mwanasaikolojia Mushobozi ni mtaalamu wa kutoa huduma za kisaikolojia na huduma zinazohusiana na maabara ya saikolojia. Pia, anatoa mafunzo ya kujengewa uwezo na kuimarishwa kimbinu kwa watu binafsi na wataalamu ndani ya Tanzania na kutoka mataifa mbalimbali duniani. Mushobozi amefanikiwa kuunda na kuandika *'psychological models'* zinazosaidia kuongoza utoaji wa huduma za kisaikolojia kupitia SNG1 na taasisi nyingine zinazotoa huduma za kisaikolojia. SNG1 inamiliki na kuongozwa na kauli mbiu yake ya kipekee isemayo, ***"AFYA YA AKILI KWA USTAWI WAKO NA VIZAZI BAADA YAKO".***

## Chagua

# *Package*

## Inayokufaa zaidi na ufurahie maisha yako ukiwa na *Afya bora ya Akili* kwa Ustawi wako na vizazi baada yako



**PACKAGES ZETU**

- CAREER VISIONARY
- STAR WARIDI
- STAR BAHARI
- STAR TALK
- STAR NEST
- STRAWBERRY STAR
- APPLE STAR
- STAR BEAUTY
- STAR CLASSIC
- ROCKET STAR
- FURNANCE STAR
- STAR OVERSHINE
- FANTASTIC STAR
- MAGIC STAR
- SPECIAL STAR
- STAR TOUCH
- WONDROUS STAR



***"WAHI SASA, WAKATI NDIO HUU"***




# CAREER VISIONARY

## T A A L U M A

*"Jenga msingi imara wa safari yako ya Kitaaluma"*

**Huduma hii inalenga kuwasaidia watu binfasi, makundi, na taasisi za kielimu kupata mwongozo wa kisaikolojia kuhusu mwelekeo wa taaluma zao. Tunatoa msaada wa kitaalamu ili kuwasaidia kuchagua njia na maamuzi sahihi ya taaluma/kazi, na kupata mafanikio kwenye maisha ya kazi.**

### Faida za Huduma hii:

- Utapata elimu ya kina kuhusu chaguo lako la taaluma (career choice)
- Utapata mwongozo wa kitaalamu ili kuchagua na kusimamia mwelekeo sahihi wa taaluma unayotaka
- Vipimo vya kisaikolojia na msaada wa kitaalamu kwaajili ya kuimarisha utendaji wako wa kazi
- Utapata ushauri wa jinsi ya kuongeza ufanisi kazini kupitia vipimo maalumu vya kisaikolojia
- Utapata Kozi za kujengewa uwezo na kuimarishwa kimbinu (Mentorship na Coaching) zinazosaidia kukuza uwezo wa kitaaluma na ustawi wa kiakili
- Utafaidika zaidi na kufahamu saikolojia ya kuishi taaluma yako pendwa

**Wanufaika:** **Wanafunzi, wafanyakazi, vikundi, taasisi za elimu, makampuni, wazazi, na watu binafsi wanaotaka kuongeza ufanisi na mafanikio kwenye taaluma zao.**

# STAR WARIDI

## U Z A L I S H A J I



*"Zalisha kwa ufanisi zaidi, ongeza tija kwako binafsi na timu yako"*

**Huduma hii inalenga kuwasaidia watu binfasi, vikundi, mashirika na viwanda kuelewa jinsi afya ya akili inavyoathiri uzalishaji. Kwa kutumia mbinu za kisaikolojia, tunatoa msaada wa kuimarisha, kuongeza na kufikia malengo ya uzalishaji kwa ufanisi mkubwa.**

### Faida za Huduma hii:

- Utapata uelewa wa jinsi afya ya akili inavyoathiri uzalishaji
- Mwongozo wa jinsi magonjwa ya kisaikolojia yanavyoathiri uzalishaji kazini
- Utajifunza namna ya kudhibiti msongo wa mawazo kazini na kuongeza ufanisi na tija kwako binafsi
- Utapata vipimo vya kisaikolojia na matibabu ya kuboresha uzalishaji kazini
- Utapata mafunzo ya namna fikra ya vizazi (generational mindset) inavyoweza kuongeza tija kazini
- Ufanisi wa kuzalisha kupitia mwongozo wa kipekee wa uzalishaji wenye afya ya akili thabiti

**Wanufaika:** **Wafanyakazi, vikundi, makampuni, viwanda, taasisi, na watu binafsi wanaotaka kuongeza na kuimarisha ufanisi wa uzalishaji na kuboresha matokeo yao kazini**



# STAR BAHARI

## M A H U S I A N O

*"Boresha mahusiano yako ili kudumisha furaha, amani ya moyo, pamoja na ustawi wako na vizazi baada yako"*

**Package hii hujumuisha huduma zinazolenga kutoa msaada wa kisaikolojia kwa watu binafsi, wenza, na wanandoa ili kuboresha afya ya akili katika mahusiano yao. Kwa kuzingatia changamoto mbalimbali za mahusiano, tunatoa ushauri na matibabu ya kisaikolojia ili kujenga misingi imara ya uhusiano wenye afya.**

### Faida za Huduma hii:

» Utajifunza ujuzi na namna bora ya kujitambua na kudhibiti hisia zako

» Utapata ushauri wa kisaikolojia kwaajili ya mahusiano kabla ya ndoa na ndoa yenyewe

» Vipimo na tiba ya kisaikolojia katika kushughulikia makovu ya kihisia na kuimarisha uhusiano wako

» Utajifunza namna mabadiliko ya kifikra na mtazamo yanavyoweza kuimarisha uhusiano wako na kizazi chako

» Utapata ujuzi wa jinsi magonjwa ya kisaikolojia yanavyoathiri mahusiano na namna ya kukabiliana nayo

» Utapata mafunzo juu ya jinsi ya kudhibiti msongo wa mawazo au sonona inayotokana na changamoto za mahusiano

**Wanufaika:** **Watu binafsi, wenza, wanandoa, familia, na vikundi vinavyohitaji msaada wa kisaikolojia katika mahusiano yao.**

# STAR TALK

## USHAURI NASIHI




***"Karibu usikilizwe, tuzungumze na upate msaada wa kisaikolojia pia"***

**Package hii hujumuisha huduma zinazolenga kutoa ushauri wa kisaikolojia kwa watu binafsi na makundi kulingana na changamoto zao. Tunatoa huduma za kitaalamu kwa kutumia mbinu mbalimbali za unasihi ili kujitambua, kudumisha ustawi wa akili na kuboresha uwezo wako wa kukabiliana na changamoto za maisha.**

**Faida za Huduma hii:**

- Utapata nafasi ya kuzungumza na kujadili kwa pamoja juu ya changamoto zinazokukabili
- Utapata ushauri wa kitaalamu kuhusu changamoto zako za maisha
- Utafaidika na darasa maalumu la kujitambua na kujua uwezo wako wa kukabiliana na changamoto
- Utanufaika na mafunzo maalumu na ujuzi thabiti wa kukabiliana na matatizo na changamoto za afya ya akili
- Utapata vipimo vya kisaikolojia kwaajili ya kutathimini na kupata ufumbuzi wa changamoto zinazokukabili

**Wanufaika:** **Watu binafsi, makundi, wanafamilia, wanafunzi, wafanyakazi, taasisi, na watu wote wanaohitaji ushauri na msaada wa kisaikolojia.**



# STAR NEST

## F A M I L I A

*"Familia ndio msingi bora wa ustawi wako na vizazi baada yako"*

**Ndani ya Package hii, utapata huduma zinazolenga kutoa msaada wa kisaikolojia kwa familia zinazokabiliwa na changamoto mbalimbali. Tunatoa huduma za kipekee za kisaikolojia ili kuboresha ustawi wa familia kwa faida ya kizazi cha leo na vizazi vinavyokuja, huku tukizingatia afya bora ya akili katika kila hatua ya mzunguko wa maisha ndani ya familia.**

**Faida za Huduma hii:**

- Familia itapata elimu kuhusu namna mzunguko wa maisha ya familia unavyoathiri afya ya akili
- Ushauri wa jinsi ya kudhibiti matatizo ya familia na kuboresha uhusiano ndani ya familia
- Matibabu na vipimo vya kisaikolojia kwa familia zenye changamoto za afya ya akili
- Mafunzo na ujuzi wa namna msongo wa mawazo na magonjwa ya akili yanavyoathiri ustawi wa familia na jinsi ya kukabiliana nayo
- Mafunzo na ujuzi thabiti wa kudhibiti migogoro na athari zake ndani ya familia na hivyo kuimarisha afya ya akili kwaajili ya kudumisha familia zenye furaha

**Wanufaika:** **Familia, wanandoa, wazazi, watoto, na jamii zinazohitaji msaada wa kisaikolojia kwa ustawi wa familia zao.**

# STRAWBERRY STAR

## V I P A J I



*"Tambua na tumia vipaji vyako kwa ustawi wa mafanikio yako na vizazi baada yako"*

Package ya Strawberry Star inalenga kuwasaidia watu binfasi kutambua, kukubali, na kutumia vipaji walivyonavyo ili kujenga maisha bora. Tunatoa msaada wa kisaikolojia na mwongozo kwa watu binafsi kutumia vipaji vyao kwa ustawi wa kiakili na kufikia malengo na ndoto zao kwa manufaa yao na vizazi vijavyo.

**Faida za Huduma hii:**

» Vipimo maalumu vya kisaikolojia ili kutambua vipaji na uwezo wako wa kipekee

» Mwongozo wa jinsi ya kutumia vipaji vyako kwa mafanikio yako binafsi na jamii

» Uelewa wa jinsi afya ya akili inavyoweza kuathiri uwezo wa kutumia kipaji/vipaji vyako

» Mafunzo ya namna fikra chanya inavyoweza kukuza vipaji na ustawi wa akili

» Kujengewa uwezo na kuimarishwa kimbinu (Mentorship and Coaching) ili kuboresha ufanisi na kuongeza tija kupitia vipaji vyako

**Wanufaika:** Watu binafsi, wanafunzi, vikundi, wafanyakazi, na jamii kiujumla wanaotaka kuboresha maisha yao kupitia vipaji walivyonavyo.



# APPLE STAR

## M I R A D I

*"Fanikisha Miradi yako kwa msaada wa mbinu za kisaikolojia"*

**Apple Star package inalenga kusaidia viongozi wa miradi na taasisi kupanga, kusimamia, na kuendesha miradi yenye mafanikio kupitia mbinu za kisaikolojia. Tunasaidia kuimarisha ustawi wa akili ili kuongeza ufanisi katika utawala wa miradi kwaajili ya maendeleo ya jamii na vizazi vijavyo.**


### Faida za Huduma hii:

- Uelewa wa jinsi afya ya akili inavyoathiri usimamizi wa miradi
- Mafunzo ya jinsi fikra ya Vizazi (generational mindset) inavyoweza kusaidia kufanikisha miradi
- Ushauri wa jinsi magonjwa ya kisaikolojia yanaweza kuathiri utendaji wa miradi
- Mbinu za kudhibiti msongo wa mawazo katika usimamizi wa miradi kwa ufanisi bora zaidi
- Utapata vipimo vya kisaikolojia na matibabu kwa timu za miradi (project teams) ili kuongeza tija na ufanisi

**Wanufaika:** **Viongozi wa miradi, taasisi, makampuni, vikundi vya kijamii, na mtu yeyote anayehusika katika usimamizi na utekelezaji wa miradi.**

# STAR BEAUTY

## U Z U R I  W A N G U



*"Tambua uzuri wako wa ndani na nje kwa ustawi wako"*

**Package hii inalenga kuwasaidia watu binafsi kuelewa na kuthamini uzuri wao wa kipekee. Tunatoa mwongozo wa kisaikolojia ili kuleta hamasa katika kujenga viwango binafsi vya uzuri wao, huku wakizingatia afya ya akili na ustawi wa vizazi vijavyo.**

### Faida za Huduma hii:

- Uelewa wa jinsi uzuri unavyohusiana na afya ya akili na ustawi wa mtu binafsi
- Vipimo vya kisaikolojia ili kusaidia kuthamini na kutambua uzuri wako binafsi
- Ushauri wa namna ya kukabili changamoto za kisaikolojia zinazosababishwa na dhana potofu za uzuri/urembo
- Mafunzo ya namna fikra chanya inavyosaidia kujenga thamani na hadhi yako binafsi
- Mwongozo wa matumizi ya teknolojia na virutubisho vya lishe kusaidia uzuri na afya ya akili

**Wanufaika:** **Watu binafsi, wanafamilia, vijana, na mtu yeyote anayetaka kuboresha fikra na mtazamo wake kuhusu uzuri na ustawi wa akili**



# STAR CLASSIC

## M E N T O R S H I P

***"Jifunze kutoka kwa waliokutangulia, jenga ujuzi wako kwa ustawi wako"***

**Star Classic ni huduma zinazolenga kutoa msaada wa kisaikolojia kupitia programu za kujengewa uwezo zenye kulenga kukuza ujuzi na uwezo wa watu binafsi katika nyanja mbalimbali za kisaikolojia. Tunatoa mwongozo wa moja kwa moja kupitia ushauri wa kipekee kutoka kwa wazoefu na waliotangulia ili kusaidia ukuaji wako binafsi.**

### Faida za Huduma hii:

» Utapata ushauri na mwongozo wa kitaalamu kutoka kwa wataalamu wenye uzoefu kulingana na taaluma yako

» Mafunzo maalumu ya jinsi ya kufikia malengo yako binafsi

» Vipimo na tathimini za kisaikolojia ili kusaidia kujenga mwelekeo sahihi wa ukuaji

» Kujengewa uwezo maalumu kwaajili ya mabadiliko ya kifikra na ustawi wa kizazi chako na vizazi vijavyo

**Wanufaika:** **Mtu binafsi, wanafunzi, wafanyakazi, vikundi, taasisi, na watu wote wanaohitaji msaada wa kisaikolojia kupitia programu za kujengewa uwezo ili kuboresha maisha na ustawi wa kiakili.**

# ROCKET STAR

## COACHING



*"Pata mwongozo sahihi, weka fikra zako kwenye njia ya mafanikio"*

**Rocket Star package ni huduma zinazolenga kuwasaidia watu binafsi kupitia programu za kuimarishwa kimbinu (coaching) zinazojikita kwenye mbinu za kisaikolojia ili kuimarisha ustawi wa akili na kufikia malengo binafsi na ya kikazi pia. Programu zetu za kuimarishwa kimbinu huchangia kubadilisha fikra na kuongeza ufanisi kwa vizazi.**

**Faida za Huduma hii:**

- Mafunzo maalumu ya jinsi ya kutumia fikra chanya ili kuboresha ustawi wa akili na mafanikio yako
- Mwongozo wa kisaikolojia kwa kutumia vipimo na tathimini za kina ili kufikia malengo binafsi na yale ya kikazi
- Programu zetu zitakusaidia kuboresha uwezo wako wa kufanya maamuzi sahihi
- Programu zetu zinazingatia ustawi wa vizazi na mafanikio endelevu

**Wanufaika:** **Watu binafsi, wafanyakazi, wanafunzi, taasisi, makampuni, na mtu yeyote anayehitaji msaada wa kuimarishwa kimbinu (coaching) kwa ustawi wa akili na mafanikio yake binafsi.**



# FURNANCE STAR

## M A L E Z I

*“Kuwa mzazi bora kwa ustawi wa watoto wako na vizazi vijavyo”*

**Package hii inalenga kutoa msaada wa kisaikolojia kwa wazazi ili kuimarisha mbinu bora za malezi. Tunatoa mwongozo na elimu ya kisaikolojia kwa wazazi ili kuhakikisha watoto wamelelewa katika mazingira yenye afya bora ya akili, hali ambayo husaidia ustawi wa kizazi hiki na vile vizazi vijavyo.**

### Faida za Huduma hii:

- Utapata elimu ya kina kuhusu athari za afya ya akili katika malezi
- Utajifuza mbinu bora za kudhibiti msongo wa mawazo unaotokana na changamoto za malezi
- Ushauri na tiba kwa magonjwa ya kisaikolojia yanayoathiri malezi bora
- Utaelimika zaidi kuhusu  saikolojia ya uchaguzi wa vifaa bora vya makuzi ya mtoto. Mfano, ni vifaa vipi umpatie mtoto wako kuchezea, n.k.
- Ushauri wa kitaalamu wa jinsi ya kukabiliana na changamoto za malezi kupitia tathimini za kisaikolojia
- Mafunzo ya namna fikra ya vizazi (generational minset) inavyoweza kuimarisha malezi bora na ustawi wa watoto

**Wanufaika:** **Wazazi, walezi, familia, na vikundi vya jamii vinavyohusika na masuala ya malezi na ustawi wa watoto**

# STAR OVERSHINE

## GENERATIONAL MINDSET



*"Jenga fikra za kizazi chenye ustawi kwa mafanikio ya leo na kesho"*

**Package hii inajumuisha huduma zenye kulenga kusaidia watu na jamii kubadilisha fikra zao kwaajili ya ustawi wa kizazi chao na vizazi vijavyo. Tunatoa msaada wa kisaikolojia ili kuwasaidia watu kuboresha fikra zao juu ya kuacha alama katika kizazi chao, huku wakizingatia afya ya akili kwa maendeleo ya kudumu.**

**Faida za Huduma hii:**


» Utapata uelewa wa jinsi afya ya akili inavyoweza kuboresha fikra zako juu ya kizazi chako na vizazi baada yako

» Utapata ushauri wa kisaikolojia ili kubadilisha fikra na kuimarisha ustawi wa vizazi

» Utapata vipimo na tathimini za kisaikolojia ili kujua mwelekeo wa fikra zako na mchango wake kwa kizazi chako

» Utapata mafunzo ya jinsi magonjwa ya kisaikolojia yanavyoweza kuathiri mawazo na fikra za kizazi, na njia bora za kuyakabili.

**Wanufaika:** **Watu binafsi, familia, vikundi, taasisi za elimu, na jamii zinazohitaji kuboresha maisha yao na ya vizazi vyao kupitia mabadiliko ya kifikra (generational mindset).**



# FANTASTIC STAR

## M A M A   M J A M Z I T O

***"Jifunze namna bora ya kukabiliana na changamoto za ujauzito kwa ustawi wa afya yako na kizazi chako"***

**Fantastic Star ni Package inayojumuisha huduma zinazolenga kuwasaidia wanawake wajawazito kushughulikia changamoto za afya ya akili wakati wa ujauzito. Kwa kutumia mbinu za kisaikolojia, tunatoa msaada ili kuhakikisha wanawake wajawazito wanapata ustawi wa akili, kwa faida yao na kizazi wanachokileta duniani.**

### Faida za Huduma hii:

- Utapata uelewa wa jinsi afya ya akili inavyoathiri ujauzito na ustawi wa mtoto
- Utanufaika na mafunzo ya jinsi ya kudhibiti msongo wa mawazo wakati wa ujauzito
- Utapata msaada na elimu ya jinsi magonjwa ya kisaikolojia yanavyoweza kuathiri ujauzito na jinsi ya kuyakabili
- Utapata vipimo na matibabu ya kisaikolojia kwaajili ya kuimarisha afya ya akili wakati wa ujauzito
- Utajifunza namna ya kutumia fikra ya kizazi (generational mindset) katika kuhakikisha ujauzito unakuwa wenye mafanikio.

**Wanufaika:** **Wanawake wajawazito, wazazi wapya, familia, taasisi za afya, vikukndi vya wanawake, na familia zinazotarajia watoto hapo baadaye.**

# MAGIC STAR

## RELAXATION



*"Pata utulivu wa akili na mwili kwa mafanikio yako na ustawi wa kizazi chako"*

**Magic Star ni Package maalumu ya kuwasidia watu binafsi na makundi kutumia mbinu za kisaikolojia kupata utulivu, kupumzika, na kujitafakari kwa manufaa ya leo na kesho. Kupata utulivu na kupumzika ni muhimu kwa afya ya akili na mwili, na tunatoa mwongozo wa kisaikolojia kwaajili ya kupunguza na kukabiliana na msongo wa mawazo na kuongeza utulivu kwa ustawi wa maisha yako ya kila siku.**

### Faida za Huduma hii:

- Utapata elimu ya kina kuhusu mbinu mbalimbali za utulivu na jinsi zinavyosaidia afya ya akili
- Utapata ushauri wa kitaalamu wa jinsi ya kuchagua mbinu sahihi za utulivu kwa maisha yako ya kila siku
- Utapata elimu ya jinsi magonjwa ya kisaikolojia yanavyoathiri uwezo wako wa kupumzika na kupata utulivu
- Utasaidiwa kufahamu namna fikra za vizazi zinaweza kuchangia katika utulivu wa akili na mwili
- Utafahamu zaidi kuhusu saikolojia ya tiba ya mazingira na utalii

**Wanufaika:** **Watu binafsi, wafanyakazi, wanafunzi, makundi ya kijamii, na watu wanaotaka kuboresha afya ya akili kupitia mbinu bora za utulivu na kupumzika.**

# SPECIAL STAR

## MATIBABU YA MUDA MREFU

*"Huduma za matibabu ya muda mrefu kwa ustawi wa afya ya akili na maisha bora"*

Special Star ni package maalumu kwa watu wenye matatizo sugu au changamoto zinazohitaji matibabu ya muda mrefu. Tunatoa matibabu ya kina ya kisaikolojia, tathmini, na vipimo vya afya ya akili kwa wale wanaohitaji msaada wa muda mrefu ili kuhakikisha ustawi wa maisha yao ya kila siku.

**Faida za Huduma hii:**

- Utapata vipimo, tathmini na mwongozo thabiti juu ya tatizo lako na namna bora ya kuendana nalo kwa ustawi wako
- Utanufaika na elimu ya jinsi afya ya akili inavyoathiri tiba za muda mrefu na ustawi wa kizazi chako na vizazi baada yako
- Utapata matibabu ya muda mrefu ya kisaikolojia kwa matatizo sugu ya akili
- Utapa mwongozo wa namna ya kutumia fikra ya vizazi (generational mindset) ili kuboresha matokeo ya matibabu ya muda mrefu

**Wanufaika:** Watu binafsi wenye matatizo sugu, familia, vikundi vya msaada wa jamii, na watu wote wanaohitaji matibabu ya muda mrefu kwa afya ya akili na ustawi wa maisha yao.

# STAR TOUCH

## M A T U K I O



***"Ongeza thamani kwenye matukio yako kwa huduma bora za kisaikolojia"***

**Package hii inahusisha kuhudhuria na kushiriki katika matukio mbalimbali yaliyopangwa na wateja wetu. Lengo ni kutoa semina, mafunzo, warsha, na ushauri wa kisaikolojia kwa washiriki waliohudhuria wenye matukio husika. Kwa kufanya hivyo, tunachangia kuimarisha afya ya akili na ustawi wa washiriki na jamii kiujumla.**

**Faida za Huduma hii:**

- Semina na mafunzo ya kina kuhusu masuala ya afya ya akili na jinsi ya kuyashughulikia
- Ushauri wa kisaikolojia na vipimo kwa washiriki wa matukio husika ili kuboresha ustawi wao
- Mafunzo ya jinsi magonjwa ya kisaikolojia yanavyoathiri mafanikio na maendeleo yetu kama jamii
- Vitabu na vifaa mbalimbali vya afya ya akili vitakavyosaidia washiriki kufaidika zaidi na shughuli iliyoandaliwa

**Wanufaika:** **Mashirika, taasisi, makampuni, vikundi vya jamii, waandaji wa matukio, na mtu yeyote anayetaka kuboresha na kunogesha matukio yake kwa huduma za kisaikolojia.**



# WONDROUS STAR

## PSYCHOLOGICAL APPLICATION OF DIFFERENT SUBJECTS

***"Tumia Hisabati, Sayansi na masomo mengine kwa mtazamo wa kisaikolojia ili kuboresha maisha yako ya kila siku"***

**Wondrous Star Package hulenga kusaidia watu kuelewa na kutumia masomo ya darasani kama vile hesabu, kemia, fizikia,na baiolojia kwa mtazamo wa kisaikolojia katika maisha yao ya kila siku. Tunatoa mwongozo wa kipekee wa kisaikolojia wa jinsi maarifa haya yanaweza kutumika kusaidia ustawi wa akili na kushughulikia changamoto za maisha.**

### Faida za Huduma hii:

- Utapata elimu ya kipekee ya jinsi ya kutumia sayansi na masomo mengine kuboresha maisha yako
- Utapata mbinu za jinsi ya kutumia maarifa ya hesabu, kemia, fizikia, baiolojia, na masomo mengine kutatua matatizo ya maisha ya kila siku
- Utapata mafunzo ya jinsi fikra za vizazi zinaweza kusaidia katika kuunganisha elimu ya darasani na maisha ya kila siku
- Matibabu na vipimo vya kisaikolojia vinavyohusisha matumizi ya sayansi katika kuboresha afya ya akili

**Wanufaika:** **Wanafunzi, walimu, taasisi za elimu, wafanyakazi, makampuni, na mtu yeyote anayevutiwa na kutumia sayansi na masomo mengine kuboresha maisha yao ya kila siku.**




**Wasiliana nasi kwa huduma bora zaidi**

Piga namba:

***+255 767 760 660***

Tunapatikana:

**IRINGA, TANZANIA.**

Tembelea mitandao yetu

*Star of New Generation1*

*www.sng1.co.tz*